**Jibu: Tusome..**

> *2Wakorintho 3:6  “Naye ndiye aliyetutosheleza kuwa wahudumu wa agano jipya; si wa andiko, bali wa roho; kwa maana andiko huua, bali roho huhuisha”.*

Kuhuisha maana yake ni “kutoa uzima/uhai”, Mungu pekee ndiye anayetoa uzima na kutupa sisi. Hivyo hapo iliposema andiko huua, bali Roho huhuisha Maana yake ni kwamba, maandiko bila ufunuo wa Roho yanaweza kuipoteza roho ya mtu na kuiua kabisa (aidha mtu huyo akafa kiroho au hata kimwili kabisa). Lakini yakitumiwa kwa uongozo wa Roho, yanampa mtu uzima, na hata kama alikuwa amekufa anaweza kufufuka tena.

Sasa tutazame ni kwa namna gani andiko linaweza kumuua mtu kimwili, na baadaye kiroho.

- **Jinsi linavyoweza kumuua mtu kimwili:**

> *Walawi 24:19 “Na mtu akimtia mwenziwe kilema; vile vile kama alivyofanya, naye atafanyiwa vivyo;*
>
> *20 jeraha kwa jeraha, jicho kwa jicho, jino kwa jino; vile vile kama alivyomtia mtu kilema, naye atalipwa vivyo”.*

> *Kumbukumbu 19:21 “Wala jicho lako lisiwe na huruma; uzima kwa uzima, jicho kwa jicho, jino kwa jino, mkono kwa mkono, mguu kwa mguu”.*

Hapo anasema **UZIMA kwa UZIMA,** maana yake ni kwamba, mtu aliyetoa uhai wa mwenzake kwa makusudi sharti na yeye uhai wake uondolewe, au kama kamvunja jino, na la kwake pia litaondolewa, kama kampiga na kumtoboa jicho, na la kwake pia litatobolewa.

Kwahiyo hili andiko na mengine mengi yakichukuliwa kama yalivyo yanaua. Na watu wengi walikuwa wanakufa kwa maandiko hayo, ilikuwa mwanamke akifumaniwa katika uzinzi, hukumu yake ilikuwa ni kifo cha kupigwa mawe mpaka afe.

Lakini Roho Mtakatifu alipokuja, aliliweka hilo sawa kwa kinywa cha Bwana wetu Yesu Kristo na kusema..

> *Mathayo 5: 38 “Mmesikia kwamba imenenwa, Jicho kwa jicho, na jino kwa jino*
>
> *39 Lakini mimi nawaambia, Msishindane na mtu mwovu; lakini mtu akupigaye shavu la kuume, mgeuzie na la pili.*
>
> *40 Na mtu atakaye kukushitaki na kuitwaa kanzu yako, mwachie na joho pia.*
>
> *41 Na mtu atakayekulazimisha mwendo wa maili moja, nenda naye mbili.*
>
> *42 Akuombaye, mpe; naye atakaye kukopa kwako, usimpe kisogo*
>
> *43 Mmesikia kwamba imenenwa, Umpende jirani yako, na, Umchukie adui yako;*
>
> *44 lakini mimi nawaambia, Wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi,*

> *45 ili mpate kuwa wana wa Baba yenu aliye mbinguni; maana yeye huwaangazia jua lake waovu na wema, huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki”.*

- **Ni kwa namna gani andiko pia linaweza kumuua mtu kiroho.**

Mfano wa andiko linaloweza kumuua mtu kiroho ni hili…

> *1Timotheo 5:23 “Tokea sasa usinywe maji tu lakini tumia mvinyo kidogo, kwa ajili ya tumbo lako, na magonjwa yakupatayo mara kwa mara”.*

Andiko hili limewapofusha watu macho na kuwafanya wawe walevi, na wasiojali  na shetani, amelipigilia msumari hili, lengo lake ni watu wafe bila kutubu ili waende jehanamu ya moto. Roho za wengi, zimekufa katika andiko hili.

Na andiko lingine ni hili.. ***Mhubiri 9:5 “kwa sababu walio hai wanajua ya kwamba watakufa; lakini wafu hawajui neno lo lote, wala hawana ijara tena; maana kumbukumbu lao limesahauliwa”.***

Andiko hili limeua watu wengi sana kiroho, na kuishia kuamini kwamba hakuna maisha baada ya kifo, na kwamba hakuna jehanamu wala kinachoendelea..Hivyo wengi kwa andiko hili, wameona ni bora kuishi maisha ya kujipenda hapa duniani, na ya kutokujali, kwasababu baada ya kifo hakuna kitakachoendelea, hata akifanya uasherati, hakuna kwenda kuhukumiwa..Hivyo wengi wamekufa na dhambi zao kwa andiko hili. www wingulamashahidi org

Bwana Yesu, Mkuu wa Uzima alisema…

> *Luka 16:19 “Akasema, Palikuwa na mtu mmoja, tajiri, aliyevaa nguo za rangi ya zambarau na kitani safi, na kula sikuzote kwa anasa.*
>
> *20 Na maskini mmoja, jina lake Lazaro, huwekwa mlangoni pake, ana vidonda vingi,*
>
> *21 naye alikuwa akitamani kushibishwa kwa makombo yaliyoanguka katika meza ya yule tajiri; hata mbwa wakaja wakamramba vidonda vyake.*
>
> *22 Ikawa yule maskini alikufa, akachukuliwa na malaika mpaka kifuani kwa Ibrahimu. Yule tajiri naye akafa, akazikwa.*

*23 Basi, kule kuzimu aliyainua macho yake, alipokuwa katika mateso, akamwona Ibrahimu kwa mbali, na Lazaro kifuani mwake.*

*24 Akalia, akasema, Ee baba Ibrahimu, nihurumie, umtume Lazaro achovye ncha ya kidole chake majini, auburudishe ulimi wangu; kwa sababu ninateswa katika moto huu.*

*25 Ibrahimu akasema, Mwanangu, kumbuka ya kwamba wewe uliyapokea mambo mema yako katika maisha yako, na Lazaro vivyo alipata mabaya; na sasa yeye yupo hapa anafarijiwa, na wewe unaumizwa.*

*26 Na zaidi ya hayo, kati yetu sisi na ninyi kumewekwa shimo kubwa, ili wale watakao kutoka huku kwenda kwenu wasiweze; wala watu wa kwenu wasivuke kuja kwetu.*

*27 Akasema, Basi, baba, nakuomba, umtume nyumbani kwa baba yangu,*

*28 kwa kuwa ninao ndugu watano, ili awashuhudie, wasije wao pia wakafika mahali hapa pa mateso.*

*29 Ibrahimu akasema, Wanao Musa na manabii; na wawasikilize wao.*

> *30 Akasema, La, baba Ibrahimu, lakini kama akiwaendea mtu atokaye kwa wafu, watatubu.*
>
> *31 Akamwambia, Wasipowasikia Musa na manabii, hawatashawishwa hata mtu akifufuka katika wafu”.*

Hapo Roho anasema kuna hukumu baada ya kifo.

Hivyo ni muhimu sana kumpata Roho Mtakatifu, wakati wa kulisoma Neno la Mungu, kwasababu bila yeye ni vigumu kulielewa Neno la Mungu na kila utakapolisoma ni rahisi kutoa tafsiri zako, na si za Roho Mtakatifu.

Kama bado hujampokea Yesu, huwezi kamwe kuyaelewa maandiko, yatakuwa ni magumu, na kila utakapoyasoma utakuwa unapata maana ambazo sio sahihi, lakini pale tu utakapoamua kufanya uamuzi wa kumpokea Yesu moyoni mwako, na ukadhamiria kutubu na kuziacha dhambi zote unazozifanya kwa wazi na kwa siri, na ukawa tayari kwenda kubatizwa katika ubatizo sahihi wa maji tele (Yohana 3:23) na kwa Jina la Yesu Kristo, siku hiyo hiyo Roho Mtakatifu ataanza kufanya kazi ndani yako na kuumba jambo jipya.

Bwana akubariki

Tafadhali washirikishe na wengine habari hizi njema, na pia kama utapenda tuwe tunakutumia mafundisho ya Neno la Mungu ya mara kwa mara kwa njia ya email yako au Whatsapp basi tutumie ujumbe kwenye namba hii +255693036618 au +255789001312 **. jiunge na channel yetu Kwa kubofya hapa >> WHATSAPP**

---

**Mada Nyinginezo:**

*JE! UMEPOKEA KWELI ROHO MTAKATIFU?*

*Kuwatema farasi, maana yake ni nini?*

Nini maana ya “Andiko huua, bali Roho huhuisha (2Wakorintho 3:6)

*Wapendwa nini maana ya hili andiko “Ushuhuda wa YESU ndio ROHO YA UNABII” (ufunuo 19:10)?*

*IFAHAMU HUZUNI NA FURAHA YA MALAIKA.*

*INJILI YA MANENO LAINI ITAKUGHARIMU.*

**Rudi nyumbani**

Share on:
WhatsApp